

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA AROBAINI NA TATU**

**03 JUNI, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA TATU – TAREHE 03 JUNI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.



III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:



IV. MASWALI YA KAWAIDA:

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

361. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY KISWAGA (MAGU):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Barabara ya Kisamba – Sayaka hadi Salama inayounganisha Mkoa wa Mwanza na Simiyu itaanza kuhudumiwa na TANROADS.

**362. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga barabara kwa kiwango cha lami kuanzia Kilosa hadi Mikumi.



**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**363. MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa Wananchi maeneo ya Hifadhi ya Kitulo ambayo hayatumiki ili wayatumie kulisha mifugo yao hususani eneo la Kwipanya.

## **WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

### **364. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini Serikali itafufua Viwanda vya Korosho vilivyopo katika Wilaya za Masasi na Newala ili kuchakata Korosho ghafi na kuongeza bei ya zao hilo.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **365. MHESHIMIWA MUSUKUMA JOSEPH KASHEKU (GEITA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Mradi wa Maji ambao ulishafanyiwa upembuzi yakinifu kwa Wananchi wa Vijiji vya Nkome, Mchangani, Katome, Nyamboge, Nzera na Rwezera.



**WIZARA YA MADINI:**

**366. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE  
(NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, nini mpango wa Serikali baada ya kukamilika kwa Mradi wa Utafiti wa Madini ya Graphite Kata ya Chiwata.

**V. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA NISHATI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
03 JUNI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**